JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAAA YA TABORa

Anuani ya ‘ MKUU WA SHULE’ SHULE YA SEKONDARI BOMBAMZINGA

Simu ya mkononi : 0785519611/0754850515. SANDUKU LA POSTA- 1075,

TABORA ,

Tarehe 15/12/2020.

KUMB NA. BSS/3116/2020

KWA MZAZI,

JINA LA MWANAFUNZI ……..

S.L. P……..

TABORA.

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BOMBAMZINGA-WILAYA YA TABORA MKOA KIDATO CHA KWANZA 2018</u>

<u>1: 0Utangulizi</u>

Ninayo furaha kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Bombamzinga ipo umbali wa kilomita (4km) kaskazini mwa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (KUTWA) katika shule ya sekondari Bombamzinga mwaka huu wa masomo 2021. Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza wwewe na mwanao sana. Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza tarehe **<u>04/01/2020</u>** na mwanao anatakiwa afike na kuripoti shuleni kwa ajili ya usajili saa mbili asubuhi siku hiyo bila kukosa.

Aidha baada ya kuipata barua hii na kuisoma kwa umakini unatakiwa kumkamilishia mwanao mahitaji yote yaliyo orodheshwa hapa chini ili kumwezesha afike shuleni kwa muda uliopangwa.

2: 0 MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA

2;1 SARE YA SHULE

- Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare/ mahitaji kama ifuatavyo

WAVULANA

I. Shati jeupe (tetroni)lenye mikono mifupi inayoishia kwenye kiwiko na lisilobana.
II. Suruali ya kijani jeshi yenye linda mbili kila upande na siwe mtindo wa modo yaan nyembamba chini(kitambaa namba moja cha suti)
III. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visigino vifupi. Haturuhusu viatu vyenye marembo
IV. Jozi mbili za soksi nyeusi.
V. Tai ya rangi ya kijani(Rangi sawa na suruali)
VI. Kwa ajili ya michezo ; Bukta , Raba rangi yoyote na traki suti ya kijani kwa ajili ya mazoezi kwa wote
VII. Suruali nyeusi kitambaaa cha suti kwa ajiliya shughuli za jioni
VIII. T-shirt maelekezo yake utayapata shuleni siku ya kuripoti.

WASICHANA

I. Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu na vinavyofunga kwa nyuzi/kamba.
II. Soksi nyeupe jozi mbili ambazo ni ndefu na hazina mistari yoyote.
III. Shati jeupe (tetroni)lenye mikono mifupi inayoishia kwenye kiwiko na lisilobana na
IV. Sketi ya kijani jeshi yenye msho mzuri malinda saizi ya kawaida na inayovuka magoti kwa wakristo na inayofunika miguu kwa waislamu.
V. Wanafunzi wa kiislam ambao kwa hiari yao watataka muonekano wa hijabu, wataatkiwa kushona nusu kanzu pia ambazo watavaaa juu na sio shati la mikono mifupi..
VI. Tai ya kijani jeshi inayofanan na kitambaa cha sketi- hii ni kwa wanovaa mashati pekee.
VII. Kwa ajili ya michezo ; Bukta , Raba rangi yoyote na traki suti pana ya kijani kwa ajili ya mazoezi kwa wote.
VIII. Sketi nyeusi ya kitambaa cha suti kwa ajili ya shughuli za jioni. Mshono uwe sawa na sketi za kijani.

2.2 Madaftari 10 (counter) quire 3 qu 4, kalamu za risasi na za wino na mkebe wa vifaa vya Hisabati(Mathematical set) Madaftari 9 ya mazoezi.

2.3 Gharama za usafiri ni juu ya mzazi ili kumsaidia kufika shuleni kwa wakati.

2.**4 Picha 2 passport size (kila mwanafunzi)**

2.5 Sweta la kijani kwa ajili ya baridi(sweta ni rangi ya kijani mgomba haifanani na suruali au sketi). Malekezo ya rangi yakikusumbua njoo uelekezwe rangi shuleni.

KUMBUKA: Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare muda wote awapo shuleni.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inatotolewa na wizara ya ELIMU sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Raisi –TAMISEMI YENYE JUKUMU LA LA USIMAMIZI WA UENDESHAJI ELIMU. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla

(b) Mahudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

© Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo.

(d) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule

(e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(g) Kutunza mali za shule.

MUHIMU: 1; mwanafunzi ataruhusiwa kutofika shuleni kwa ajili ya ugonjwa na vielelezovya kuumwa kwake view vimethibitishwa au amepata msiba wa mzazi, mlezi ama ndugu aliyeko karibu. Taarifa za msiba ziletwe moja kwa moja kwa mkuu wa shule

2. Mzazi anatakiwa kufuatilia ripoti zifuatazo

I. Matokeo ya mitihani
II. Maendeleo ya kitaaluma

Wakati wote mwanafunzi akiwa shuleni, mwanafunzi anapaswa kuzingatia sheria zote za shule ili kuweza kudumisha amani na uelewano na wanafuzi wenzake na kati ya shule na jamii inayomzunguka. Hivyo itamlazimu mara tu afikapo shuleni azisome sheria na kanuni za shule na kuzielewa na kuzitekeleza kwa uaminimfu mkubwa.

Makosa yafuatayo yanaweza kumsababishia mwanafunzi kufukuzwa shule hata kama atakuwa ametenda kosa hili kwa mara ya kwanza:

1. **Wizi**
2. **Utoro wa Shule**
3. **Kupigana au kupiga**
4. **Ulevi, uvutaji wa bangi, na matumizi ya madawa ya kulevya**
5. **Fujo, Migomo, Kuchochea na Kuongoza au Kuvuruga Amani na Usalama wa watu.**
6. **Kudharau Bendera ya Taifa**
7. **Makosa ya Jinai**
8. **Kuoa au Kuolewa**
9. **Kuharibu mali ya umma kwa makusudi**
10. **Kupata, kusababisha au kutoa mimba kwa msichana ndani au nje ya shule**
11. **Uasherati, Ubakaji na Ushoga**
12. **Kutukana Mwalimu, Wafanyakazi wasio Walimu, Viongozi wa Wanafunzi au mtu mwingine yeyote.**
13. **Kugomea adhabu halali ya Mwalimu au ya Kiranja wa Shule**
14. **Kumiliki Simu au kukutwa na Simu ndani ya eneo la Shule.**
15. **Kuacha kufanya jaribio, mtihani au jaribio bila taarifa yeyote**
16. **Kuishia njiani**

4. 0 MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA

Fomu ya kupimwa afya yake(Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara afikapo shuleni.

Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kama hana ajaze fomu ya uthibitisho wa uraia (AFFIDAVIT FORM)

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kyatekeleza kikamilifu.

UTHIBITISHO WA URAIA

AFFIDAVIT FORM:

Date and place of birth .....(Capital letters)

Full Name .....

(Postal and residential; address)

Aged ..... do solemnly and sincerely declare as follows:

1. That I am father/mother near relative of (clear bother) (state full names)

2.That the said.....was born ..... in the village/town of..... in ..... District of Tanzania.

3. That I remember the occasion as I was presently after his /her birth I the said ..... make

This declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the Oaths (judicial proceeding and statutory declarations act ,1966.

....

Revenue Signature of the person making the Declaration

.....

Magistrate /commissioner for For this Declaration is made and subscribed by the said

.....

Who is well known to me personally this ..... Day of

Signature ..... qualification .....

(Official rubber stamp)

Address.....

.....

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

BOMBAMZINGA SECODARY SCHOOL

P.O.BOX 1075.

TABORA

.....

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

This form must be completed by a Government Medical Officer.

Student's full name: .....

Present age .....

Blood Test .....

Stool Examination:.....

T.B. test: .....

Asthma:.....

Eye Disorder: .....

Nose disorder:.....

Ear Disorder:.....

Skin Disease:.....

Anaemia:.....

Chest: .....

Operations: .....

Serious Accidents:.....

Any other infections disease:.....

Pregnancy:.....

Additional information e.g. Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc.....
.....
.....

I certify that I have personally examined Mr./miss ..... and found him/her fit un-fit to pursue studies

Signature .....

Designation .....

(Official rubber stamp) .....

FOMU YA MAKUBALIANO

1. **SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ……nimeyasoma na kuyaelewa maagizo pamoja na mwongozo wa mambo ya kuzingatia shuleni. Ninaipokea nafasi hii niliyopewa na Taifa kuwa mwanafunzi wa kutwa wa Shule ya Sekondari Bombamzinga na nna ahidi kuzitekeleza Sheria na Kanuni za Shule na kuzingatia masomo yangu kama inavyotakiwa kinyume chake nichukuliwe hatua zinazostahili.

Sahihi……. Tarehe……

2. **SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi…….Mzazi/Mlezi wa ……nimeyasoma maagizo haya na kujadiliana na mwanangu. Nimeikubali nafasi hii aliopewa mtoto wangu na nitamtimizia mahitaji yake yote kama mwanafunzi wa kutwa. Aidha nitahakikisha muda wote anazingatia Sheria na taratibu za shule.

Sahihi…….. Tarehe…….

MWISHO

NAKUTAKIA SAFARI NJEMA KUJA SHULENI BOMBAMZINGA SEKONDARI-KARIBU SANA. NI TUMAINI LETU KWAMBA MWANAO ATAFURAHIA NA KUJIVUNIA SHULE YAKE MPYA

……

M.M. MACHIBULA

MKUU WA SHULE